**MWANDISHI: JULIETH J. MWIHAMBI**

**PHONE: +255 757 761162**
***Email: info@abigaminzaresearch.co.tz***

Mwanamke ni nguzo muhimu sana katika kuleta maendeleo ya jamii na taifa lake katika nyanja ya uchumi, afya, na maadili mema.

Mwanamke wa Tanzania ni nguzo kwa maendeleo ya Jamii na Taifa lake, pale anapoamua kujihusisha kwa bidii, kujituma kwa nguvu na uwezo wake, na kwa kutumia maliasili na lasirimali zinazopatikana mahali alipo ili kuleta maendeleo ya familia yake.

Mwanamke wa Tanzania atakapo amua kujituma pale pale alipo iwe ofisini, shambani, katika biashara nyumbani kwenye shughuli za ujasiriamali na katika kutoa huduma mbalimbali zilizo halali, maendeleo ya Jamii hupatikana kwa haraka na kwa wepesi.

Mwanamke anategemewa katika ngazi ya familia kuleta maendeleo kutokana na uwezo wake wa asili aliopewa na Mwenyezi Mungu, pamoja na ufunifu utaalamu alionao, katika kuleta maendeleo ya kiuchumi, afya, (ya akili, mwili na roho) na pia katika kuboresha na kuimarisha maadili meme ya Jamii yake na Taifa kwa ujumla.

Mwanamke usingoje kesho, sasa ndio wakati muafaka wa kuamua kuamka na kuanza kujituma kuchangia uwezo ulio nao, ki elimu, ujuzi na rasilimali alizonazo, kutumika katika kuharakisha kuleta maendeleo ya Jamiii na Taifa kwa ujumla.

Makala hii ina lengo la kuwahamasisha wanawake wa Tanzania katika kuongeza kujitahidi, kujitoa, kujibiidiisha na kujituma kwa hali na mali katika shughuli za kuleta na kuongeza kiwango cha maendeleo ya kiuchumi, afya (ya akili, mwili na roho), na maadili mema, katika kila Jamii ya mwanamke husika, na hatimaye kuleta maendeleo hayo kwa Taifa zima kwa ujumla.

## Mwanamke katika kuleta maendeleo ya kiuchumi Jamii na Taifa lake.

Mwanamke anauwezo mkubwa wa kuinua pato la familia na kuiwezesha familia kuinua uchumi wake pale ambapo ataamua kwa dhati kujituma kwa bidii na kuwa tayari kujitoa na kutumia ujuzi, uzoefu, utaalamu, elimu na rasilimali alizonazo kwa lengo la kuinua na kuongeza kipato kwa familia yake. Kila mmoja kwa nafasi yake. Mfanyakazi, fanya kazi kwa bidii na maarifa, mkulima kwa bidii na maarifa, mfanyabiashara na mjasiriamali pia, kila mmoja atakapo jitahidi na kujituma, bila

kujiwekea vikwazo mwenyewe kwa kisingizio cha kuwa na elimu ndogo, ujuzi mdogo na rasilimali duni.

Jitahidi kwa kile ulichonacho na utafanikiwa kuongeza kiwango cha kipato kwa familia yako. Kila mmoja akifanikiwa katika familia yake Jamii na Taifa litafanikiwa.

“Ufike wakati jamii iwaamini wanawake kwa sababu wanauwezo mkubwa wa kujenga uchumi imara kwenye nyakati ngumu Mama Anna Elisha Mghwira (2015)”.

‘Jamii zote hunufaika pale ambapo wanawake wana afya njema, wapo salama na wanaweza kuchangia nguvu zao, uongozi na ubunifu wao katika kujenga uchumi wa dunia. John Fo Kerry (2013)”

**Mwanamke katika kuboresha na kuimarisha afya (ya akili, mwili na roho), katika familia na jamii yake.**

Mwanamke anao wajibu na uwezo wa kuiwezesha familia yake kuwa na afya bora, kwa kupangilia aina na muda wa mlo kwa kila siku, usafi wa mazingira, usafi wa ndani na nje ya nyumba na pia kusimamia usafi binafsi wa kila alie katika familia yake, pia anao uwezo wa kuhimiza wanajamii wake kufanya mazoezi kwenda katika nyumba za ibada, na kwenda clinik pale wanapo hitajika. Atakapofanikiwa katika hilo, ataiwezesha familia yake kuwa na afya bora ya akili, mwili na roho, kisha wanfamilia watakuwa na nafasi nzuri ya kufanya shughuli za kuzalisha mali na kujiongezea kipato.


**Mwanamke katika kuleta na kuimarisha maadili mema ya wanajamii yake.**

Kwa kutumia uwezo aliopewa na Mwenyezi Mungu, elimu aliyonayo ujuzi na ufahamu wake, wmanamke anaweza kuongoza familia na jamii yake katika maadili mema, kuepusha ulevi, utumiaji wa madawa ya kulevya uvivu, utoro na mengine mengi yasiyofaa.

Mwanamke atafanikiwa iwapo atajitoa kwa moyo na kutumia uwezo alionao, ushawishi na nguvu ya asili ya umama katika ngazi ya familia, hapo vijana wengi wanajamii yake watakapo kuwa na maadili mema, wataweza kujituma nakufanya kazi kwa bidii na maarifa na kisha kuleta maendeleo katika ngazi ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla.

“Kama ilivyo katika nchi yetu, matatizo makubwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yanayoikabili dunia yetu, hayataweza kutatuliwa bila ushiriki kikamilifu wa wanawake.” John F. Kerry (2013).

Mfumo wa dhana: Mwanamke ni nguzo muhimu katika kuleta maendeleo Tanzania




Source:- Julieth J. Mwihambi (2016).

Wakati muda unakimbia kwa kasisana, ni muhimu mwanamke wa Tanzania kuamua kujibidiisha, kujituma kwa nguvu, uwezo, mali, elimu na kwa rasilimali ndogo iliyopo ili kuimarisha na kuongeza uchumi, afya na maadili mema ya jamii yake, na jamii hii inapofanikiwa ndipo pia Taifa zima litafanikiwa.

"Wanawake tukiamua tunaweza."

Reference;

1. Nguvu na maarifa ya mwanamke kiuchumi. Mama Anna Elisha Mghwira (2015) www.jamiiforum.com
2. Kwanini wanawake ni muhimu katika sera za Marekani. John F. Kerry (2013) Tanzania.usembassy.gov



Julieth J. Mwihambi , January 2019
Mwandishi